JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# SHULE YA MSINGI MARTIN LUTHER

P. O. Box 1786 Dodoma. Tel. +255 26 2395029, +255 784 449098
Fax +255 26 2395030 (www.martinlutherschooldodoma.sc.tz)

*"Elimu bora zaidi kwa kizazi kipya"*

## DARASA LA III

## HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

## KAZI YA NYUMBANI – JUNI 2026

**JINA LA MWANAFUNZI: ______________________________**

## MAELEKEZO

1. **Kumbuka kuandika majina yako matatu kwa usahihi.**
2. **Jibu maswali yote kulingana na maelekezo.**
3. **Soma maswali kwa ufasaha kabla ya kujibu.**
4. **Kazi hii inapaswa kurudishwa shuleni pindi tu shule itakapofunguliwa.**

**JINA: ________________________________________DARASA III: ___________**

**Chagua herufi ya jibu sahihi miongoni mwa machaguo uliyopewa kisha uandike herufi ya jibu hilo katika kisanduku kilichowazi.**

**1.** Biashara ya utumwa ilianza mara tu baada ya wageni kutoka nchi za uarabuni kuja hapa nchini, ambapo soko kuu la biashara hii lilikuwa ni;
A. Zanzibar  B. Tanga  C. Kilwa  D. Bagamoyo  [ ]

**2.** Katika eneo la Tendaguru – Lindi paligundulika mabaki ya mjusi mkubwa duniani aitwae Dinosaria na mabaki hayo kuchukiliwa na kupelekwa nchini Ujerumani. Je, uvumbuzi huo ulitokea mwaka gani?
A. 1999  B. 1906  C. 1959  D. 1996  [ ]

**3.** Miongoni mwa urithi wa kihistoria tulionao hapa nchini ni nyayo za binadamu wa kale zinazopatikana eneo la Laetoli – Ngorongoro – Arusha. Je, nyayo hizo zinaaminika zipo tangu miaka mingapi iliyopita?
A. 1,500,000  B. 2,800,000  C. 3,700,000  D. 3,400,000  [ ]

**4.** Ni sehemu ya maneno yaliyokopwa kutoka katika lugha ya kiarabu na kuwekwa katika lugha ya Kiswahili.
A. Dunia  B. Gunia  C. Pesa  D. Shikamoo  [ ]

**5.** Ni eneo ambalo ni sehemu ya urithi hapa nchini na umaarufu wake unatokana na uwepo wa michoro ya mapangoni.
A. Kondoa – Irangi – Dodoma  B. Olduvai – Arusha  [ ]
C. Kunduchi – Dar-es-Salaam  D. Laetoli – Arusha

**6.** Hustoria ya Tanzania imeundwa na matukio mbalimbali ambayo yalitokea kipindi cha nyuma. Je, ni tukio gani lilitokea mnamo mwaka 2002?
A. Vita ya majimaji  B. Ajali ya treni – Dodoma  [ ]
C. Kifo cha Nyerere  D. Uvumbuzi wa Dinosaria

**7.** Kusalimiana ni mojawapo ya matendo ya kimaadili katika jamii. Watu walisalimiana kwa mitindo ifuatayo ISIPOKUWA;  [ ]
A. Kusimama  B. Kupiga magoti  C. Kusikiliza masimulizi  D. Kushikana mikono

**JINA: ________________________________________DARASA III: ___________**

**8.** Maadili ni mwenendo au utendaji uliokubalika katika jamii. Miongoni mwa matendo yafuatayo nit endo lipi halifai katika jamii?
A. Kuwatembelea wagonjwa B. Kusema ukweli [ ]
C. Kuwasaidia wengine D. Kutoa na kupokea rushwa

**9.** Jamii zilizoishi maeneo ya Pwani ya bahari ya Hindi wakati wa biashara na watu kutoka mashariki ya mbali na kati walirithi tamaduni za kigeni kama vile;
A. Dini ya kiislamu B. Dini ya kikristo C. Makanisa D. Shule [ ]

**10.** Kitendo cha kutoa au kupokea fedha au kitu cha thamani ili kutenda kinyume na haki ya mtu mwingine huitwa;
A. Utumwa B. Rushwa C. Haki D. Wajibu [ ]

**11.** Aina ya urithi unaohusu masuala ya kijamii yaliyorithiwa kutoka vizazi vilivyopita ambayo hayawezi kushikika au kuonekana ni; [ ]
A. Urithi B. Magofu C. Urithi usioshikika D. Urithi unaoshikika

**12.** Urithi wa bidhaa kama sahani na shanga zilizoletwa na wageni kutoka mashariki ya mbali na kati hupatikana; [ ]
A. Kilwa B. Zanzibar C. Arusha D. Bagamoyo

**13.** Kumbukumbu ya matukio yaliyotokea zamani za kale katika jamii zetu huitwa; [ ]
A. Historia B Urithi C. Maadili D. Historia ya Tanzania

**14.** Ni jumba lililokuwa ikulu ya Sultani wa Kilwa.
A. Caravan – Serai B. Husuni – Kubwa C. Msikiti mkuu D. Kunduchi [ ]

**15.** Eneo la Oldupai – Arusha kuligunduliwa fuvu la binadamu wa kale. Je, fuvu hilo liligunduliwa mwaka gani?
A. 1906 B. 1900 C. 1959 D. 1961 [ ]

**16.** Miongoni mwa aina zifuatazo za mavazi ya asili ni vazi gani huvaliwa na jamii ya Wamaasai?
A. Kupilo B. Kishade C. Mgolole D. Lubega [ ]

**JINA:** ______________________________________**DARASA III:** ___________

**17.** Kila jamii ina taratibu, kanuni, sheria na miongozi ambayo kama wanajamii wamekubaliana kuifuata na kuitii. Je, miongozo, sheria, kanuni na taratibu zilizopo katika jamii huitwa;
A. Utamaduni B. Urithi C. Kanuni D. Utandawazi [ ]

**18.** Urithi wa asili hujumuisha vitu au maumbo mbalimbali ya kuvutia na kustaajabisha ambayo huunda sura ya nchi. Je, miongoni mwa mambo yafuatayo ni jambo gani huunda sura ya nchi?
A. Sanaa B. Milima C. Ufundi D. Maarifa [ ]

**19.** Tanzania ni nchi ambayo ina urithi mwingi wa asili na wa aina tofauti tofauti. Miongoni mwa maziwa yafuatayo ambayo ni sehemu ya urithi wa asili ni ziwa gani refu kuliko maziwa yote duniani?
A. Ziwa Nyasa B. Ziwa Viktoria C. Ziwa Tanganyika D. Ziwa Eyasi [ ]

**20.** Mbuga ya Serengeti ni mbuga ambayo hupatikana katika mikoa ya Mara na Arusha, pia hufika mpaka nchi jirani ya Kenya ambapo huko huitwa?
A. Serengeti B. Maasai Kenya C. Simba safari D. Maasai Mara [ ]

**21.** Mlima mrefu Zaidi hapa barani Afrika hupatikana nchi gani?
A. Tanzania B. Kilimanjaro C. Kenya D. Malawi [ ]

**22.** Madini ni sehemu ya urithi wa asili ambao Tanzania imebarikiwa nao. Miongoni mwa madini yafuatayo ni madini gani hupatikana Tanzania pekee?
A. Chumvi B. Tanzanaiti C. Chuma D. Dhahabu [ ]

**23.** Tanzania ni nchi ambayo imeundwa na jamii zenye makabila mbalimabli Zaidi ya 120. Je, kabila la Wamakonde hupatikana katika mkoa gani?
A. Mwanza B. Tanga C. Mtwara D. Mbeya [ ]

**24.** Visiwani Zanzibar kuna mbuga ya Wanyama ya Jozani ambayo ni mbuga pekee inayopatikana katika visiwa hivyo. Je, mbuga hii ni maarufu kwa aina gani ya Wanyama? [ ]
A. Simba B. Tembo C. Swala D. Mbega wekundu

**25.** Msingi wa utamaduni ambao huhimiza watu kuungana na kufanya jambo au kazi kwa pamoja na umoja ili kuleta ufanisi Zaidi ni;
A. Ushirikiano B. Tabia njema C. Mavazi D. Kuheshimiana [ ]

**JINA: ________________________________________DARASA III: ___________**

**Oanisha maneno kutoka KIFUNGU “A” na KIFUNGU “B” ili kuleta maana kamili.**

| KIFUNGU “A” | MAJIBU | KIFUNGU “B” |
|---|---|---|
| **26.** Kuomba fedha au zawadi ili kufanya jambo fulani | [ ] | A. Uhusiano |
| **27.** Jumba la wafanya biashara ya utumwa | [ ] | B. Adumu |
| **28.** Dini, mila, maarifa na elimu ya jadi | [ ] | C. Kumnyima mtoto chakula |
| **29.** Mdundiko | [ ] | D. 10.12.1963 |
| **30.** Uhuru wa Tanganyika | [ ] | E. Ngoma ya Wagogo |
| **31.** Sehemu ambayo nyaraka za kihistoria hutunzwa | [ ] | F. Wajibu wa mtoto |
| **32.** Huelezea matendo yanayofaa na yasiyofaa katika jamii | [ ] | G. Vyanzo vya historia |
| **33.** Muungano wa Tanganyika na Zanzibar | [ ] | H. Mabonde |
| **34.** Bugobogobo | [ ] | I. Wamisionari |
| **35.** Kifo cha Mwl. Nyerere | [ ] | J. Haki |
| **36.** Maeneo yenye historia ya utumwa | [ ] | K. Butiama – Mara |
| **37.** Makanisa yaliyojengwa na wamisionari | [ ] | L. Wangoni |
| **38.** Jambo au mambo ambayo mtu anapaswa kuyafanya au kuyatimiza | [ ] | M. Wajibu |
| **39.** Lizombe | [ ] | N. Azania front |
| **40.** Makumbusho ya Mwl. Nyerere | [ ] | O. Bagamoyo na Zanzibar |
| **41.** Jambo au kitu chochote unachostahili kuwa nacho kwa mujibu wa sheria | [ ] | P. 14.10.1999 |
| **42.** Wageni kutoka Ulaya | [ ] | Q. Wasukuma |
| **43.** Isimila – Iringa na Olduvai – Arusha | [ ] | R. 26.04.1964 |
| **44.** Kusikiliza masimulizi na vyombo vya habari | [ ] | S. Maadili |
| **45.** Kufanya kazi ndogondogo | [ ] | T. Makavazi |
| **46.** Sansa | [ ] | U. 09.12.1961 |
| **47.** Uhuru wa Zanzibar | [ ] | V. Wazaramo |
| **48.** Matendo yanayokiuka haki za mtoto | [ ] | W. Urithi usioshikika |
| **49.** Ngoma ya asili ya Wamaasai | [ ] | X. Caravan – Serai |
| **50.** Hali ya watu kuwa na ufungamano katika jamii | [ ] | Y. Rushwa |
| | | Z. Ushirikiano |

**JINA: ________________________________________ DARASA III: ___________**

**Chagua jibu sahihi kwenye mabano kisha andika kwenye nafasi iliyoachwa wazi.**

**51.** Wafanyabiashara wa biashara ya utumwa walitoka nchi za _____________________ (Afrika, Ulaya, Uarabuni)

**52.** Wageni kutoka Ulaya walituachia urithi wa mazao mbalimbali kama vile __________________ (karafuu, mihogo, iliki)

**53.** Sehemu ya maeneo yaliyokopwa kutoka lugha ya kihindi na kuwekwa katika lugha ya Kiswahili ____________________ (marahaba, dunia, mwalimu)

**54.** Wamisionari walikuja nchini kwa lengo la kueneza dini ya ______________ (kiislamu, kihindu, kikristo)

**55.** Miongoni mwa maadili yanayosisitizwa katika jamii zetu ni pamoja na _____________________________ (kupenda kufanya kazi, kuiba, kutoa rushwa)

**56.** Ni elimu kuhusu matukio yaliyotokea nchini Tanzania tangu mwanzo wa maisha ya watu mpaka sasa ___________________________________ (historia, urithi, historia ya Tanzania)

**57.** Kupata taarifa za kihistoria kupitia habari na simulizi zilizoandikwa kwenye vitabu huitwa ________________________________ (masimulizi, kusoma vitabu, tovuti)

**58.** Mwana akiolojoa aliyevumbua fuvu la zamadamu huitwa ____________________________ (Dkt Patric Kamanga, Dkt Louise Leakey, Dkt Alberto Mwanitu)

**59.** Mfumo ambao binadamu alitumikishwa bila malipo na kumilikiwa na mtu mwingine huitwa _______________________ (utumwa, utumishi, wajibu)

**60.** ____________________________________ urithi wa asili unaoshikika. (zana za kale, milima, magofu)

**Chagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku hapo chini kisha uandike jibu hilo kwenye nafasi iliyoachwa wazi.**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Udhalilishaji,** | **Ukatili,** | **Unyanyasaji,** | **Maadili,** | **John P. Magufuli,** |
| **Engaruka – Arusha,** | **Ziwa Nyasa,** | **Mlima Kilimanjaro,** | **Ziwa Viktoria** | |

**61.** Ziwa namba nane kwa ukubwa duniani ni _________________________________________________

**JINA:** ________________________________________ **DARASA III:** ___________

**62.** ________________________________________ ni kitendo cha kufanyiwa matendo ya kuaibishwa.

**63.** Matendo ya kuumiza, hali ya mateso na maumivu dhidi ya mtu mwingine kwa makusudi __________

**64.** Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania ____________________________

**65.** Eneo lenye magofu ya miundombinu ya umwagiliaji ______________________________________

**Chunguza matendo katika jedwali yanayohusu haki na wajibu wa mtoto. Weka alama ya vyema (✓) katika sehemu ya haki kama tendo ni la haki na sehemu ya wajibu kama tendo ni la wajibu.**

| MATENDO | HAKI | WAJIBU |
|---|---|---|
| **66.** Kuwasalimia watu wengine na waliokuzidi umri | | |
| **67.** Kupata mahitaji ya shule, chakula na malazi | | |
| **68.** Kushirikishwa kufanya maamuzi | | |
| **69.** Kuwathamini watu wenye mahitaji maalumu | | |
| **70.** Kupata nafasi ya kucheza | | |
| **71.** Kupata malezi bora | | |
| **72.** Kuheshimiwa na watu wengine | | |
| **73.** Kulindwa | | |
| **74.** Kufanya kazi zinazoendana na umri wake | | |
| **75.** Kupata elimu bora | | |

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika majibu sahihi.**

**76.** Vitendo vya rushwa huweza kufanyika katika maeneo mbalimbali kama vile;

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________

**77.** Jamii zetu zinasisitizwa kuwasaidia watu wengine na kusaidia watu wenye mahitaji maalumu. Taja makundi mawili (2) yenye uhitaji maalumu.

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________

**78.** Orodhesha magofu mawili (2) yaliyojengwa na watu kutoka mashariki ya mbali na kati.

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________

**JINA:** ______________________________________________**DARASA III:** ____________

**79.** Kutoa taarifa pindi unapoona vitendo vya rushwa ni njia mojawapo ya kuzuia na kupambana na rushwa. Ni sehemu gani unaweza kutoa taarifa juu ya uwepo wa rushwa?

i) ________________________________________

ii) ________________________________________

**80.** Chombo kilichoundwa na serikali ili kuzuia vitendo vya rushwa kinaitwa ______________________

**81.** Kila jamii ina utamaduni wake wa namna ya kuishi na kutenda, jamii moja hutofautiana utamaduni na jamii nyingine, hasa katika mavazi. Orodhesha aina mbili (2) za mavazi ya asili.

i) ________________________________________

ii) ________________________________________

**82.** Wajibu wa mtoto umegawanyika katika sehemu mbili (2) ambapo mtoto anao wajibu anapokuwa shuleni na nyumbani. Je, ni wajibu gani alionao mtoto akiwa nyumbani?

i) ________________________________________

ii) ________________________________________

**83.** Orodhesha matukio mawili yanayounda historia ya Tanzania.

i) ________________________________________

ii) ________________________________________

**84.** Jamii za kale ziliweza kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kijamii. Taja shughuli ambazo jamii za kale ziliweza kushirikiana.

i) ________________________________________

ii) ________________________________________

**85.** Orodhesha umuhimu wa kujifunza somo la historia ya Tanzania na madili.

i) ________________________________________

ii) ________________________________________

**JINA:** ________________________________________**DARASA III:** ___________

**Chunguza picha ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.**



**Maswali**

**86.** Picha hapo juu inaonesha mabaki (magofu) ya jengo gani? __________________________

**87.** Jengo hilo lilijengwa katika mji gani? _________________________


**88.** Je, jengo hilo katika picha lipo katika aina gani ya urithi? ____________________________

**89.** Jengo hilo lilijengwa na watu kutoka mataifa ya ukanda upi? _________________________

**90.** Taja jaengo lingine ambalo lilijengwa katika mji ambao jengo hapo juu katika picha hupatikana _______

**JINA: ________________________________________ DARASA III: ____________**

**Chunguza kielelezo kifuatacho kisha jibu kwa kujaza nafasi zilizowazi.**




**Soma kwa makini sentensi zifuatazo zinazoeleza mtiririko wa viongozi wa juu wa Tanzania, kisha panga sentensi hizo kwa mtiririko kuanzia na sentensi inayoelezea kiongozi wa kwanza hadi wa sasa kwa kuandika herufi A – F.**

**95.** Benjamini Wiliam Mkapa aliiongoza Tanzania kwa miaka 10 mara baada ya Ali Hassan Mwinyi kuanzia mwaka 1995 – 2005. **[ ]**

**96.** Kuanzia mwaka 2005 mpaka 2015, Rais wa Tanzania alikuwa ni Jakaya Mrisho Kikwete ambae pia aliiongoza kwa miaka 10. **[ ]**

**97.** Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliongoza Tanzania kwa miaka 21 kuanzia mwaka 1964 hadi mnamo mwaka 1985. **[ ]**

**98.** Kuanzia mwaka 2021 mpaka sasa Rais anaeiongoza Tanzania ni Samia Suluhu Hassani. **[ ]**

**99.** Ali Hassani Mwinyi aliiongoza Tanzania kwa miaka 10 mara baada ya Mwl Nyerere kuanzia mwaka 1985 mpaka 1995. **[ ]**

**100.** John Pombe Magufuli ndiye Rais aliyeiongoza Tanzania kwa muda mfupi zaidi, aliongoza kwa miaka saba (7) tu kuanzia 2015 hadi 2021 ambapo alifariki. **[ ]**